


Ukweli Hauna Kutu

Pambazuko

Toleo Namba 014

Jumatatu Oktoba 10-16, 2022

Toleo Maalum la Miaka 23 Bila Nyerere



**Wanajeshi
wamtikisa
Nyerere**

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tuzienzi daima tunu za Nyerere

OKTOBA 14, kila mwaka ni siku ambayo Taifa linaadhimisha kumbukizi ya kifo cha Baba wa Taifa letu na aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

M w a l i m u Nyerere alifariki dunia Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mt. Thomas iliyopo London, Uingereza alipokuwa akiendelea kupatiwa matibabu. Ilibainika kitabibu kwamba Mwalimu alipatwa ugonjwa wa saratani ya damu.

Wakati wa uhai wake, Mwalimu aliyongoza Tanganyika na baadaye Tanzania alipata sifa za kuwa kiongozi mwenye kujali utu, kuzingatia katiba na zaidi sana kuwa na uzalendo usiotiliwa shaka ya aina yoyote.

Mwalimu Nyerere hakupata sifa lukuki kwa kujipendekeza kwa “wakubwa” wala kuonea watu, hapana! Alijenga mizizi ya sifa zake za uongozi kwa kutenda haki, kujali misingi ya utu na kuikumbatia Katiba ya Tanzania, hata kama ilikuwa na “mashimo” mengi.

Mwalimu Nyerere katika kuitumikia nchi changa, kwa misingi hiyohiyo ya uzalendo, alichukua hatua kadhaa ambazo hazikupendeza, lakini alikuwa na sababu nzuri za kufanya hivyo.

Sababu hizo hazikuwa na mizizi ya kuonea, kupendelea kundi Fulani au kujijengea wigo wa kuiba mali za umma kwa manufaa binafsi na familia zake.

Ni Mwalimu Nyerere ambaye alikataa kuona tabaka moja linanyonya tabaka jingine; iwe ni katika ajira, kufanya biashara na hata katika maisha mengine. Alitamani kuona kila mmoja

akifurahia uhuru wa nchi yetu uliopatikana kwa jasho na hata damu.

Baada ya miaka yake ya kuongoza - akiwa ameitumikia nchi kwa miaka 24, aliamua kung’atuka ili kuacha wengine waongoze naye akibaki kuwa mshauri.

Ni hakika kuwa Mwalimu Nyerere alikuwa mwana shababi wa Tanzania na Afrika ambaye alihakikisha usawa, uhuru na maendeleo yanalindwa kwa nguvu zote.

Hata hivyo, isivyokuwa bahati, baada ya Mwalimu kufariki dunia, Tanzania ikaanza kupata sifa mbaya ambazo hazikuwahi kuwepo wakati wa uongozi wa muasisi huyo.

Kutokuwepo kwake, kukaanza kushuhudiwa kuwepo kwa dalili za ukabila, kuongezeka kwa rushwa, matumizi mabaya ya madaraka na ufisadi wa kupindukia.

Uzalendo ukaonekana kuwa “bidhaa” adimu, kwani watu wengi, hasa viongozi wengi walioaminiwa na umma wakageuka kuwa walafi na wakwapaaji wakubwa wa mali za umma.

Undugunaizesheni, umimi na ukabila ukaonekana kutamalaki na kibaya zaidi ukifanywa bila kificho na hali hiyo ikakomaza majanga mengine na kuimarisha mnyororo wa wizi na ufisadi katika ofisi za umma.

Sasa basi, wakati Tanzania inaadhimisha miaka 23 bila ya kuwa na Mwalimu Nyerere, ni wakati muafaka wa kila mwananchi kutafakari namna ya kumuenzi muasisi huyo na mwana wa Afrika kwa kukataa na kukemea madhila yote yanayofifisha uzalendo.



Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: pambazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



“Mtu mwenye hekima hujifunza kwa makosa ya wengine, mpumbavu kwa makosa yake mwenyewe.” - Mithali ya Kilatini

Uasi wa Mwalimu Nyerere

Na Shaaban LULELA

MUASISI wa Tanganyika na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alikuwa muasi. Alipenda uasi na alikuwa tayari kuusimamia uasi wake mbele ya mtu au taasisi yoyote.

Hakujali wanamuonaje ilimradi aliamini kile alichuamini na hakuyumba wala kuyumbishwa. Alipenda kusikiliza nafsi na matamano yake.

Katika uasi wake, akipata nafasi, alikuwa akiuelezea na kuufafanua, lakini hakuzuia mawazo ya watu wengine na alipokea hata ushauri kwa baadhi ya mambo.

Hata hivyo, katika kupokea ushauri, alikuwa akiuchambua na kupima endapo unabeba mashiko zaidi ya imani yake – endapo ataona “mwepesi,” anaachana nao na anasonga mbele na kile anachoamini.

Katika kusimamia kile alichuamini, Mwalimu hakufanya hivyo kwa ajili ya tumbo lake, wala familia yake, la hasha! Aliangalia umma na namna unavyoweza kupata afueni ya maisha kwa kupokea ushauri nje na mtazamo wake.

Ni kutokana na msimamo wake usioyumba, alipachikwa majina kadhaa ikiwamo “Haambiliki,” – kwamba wengi waliamini ni kiongozi asiyesikiliza “la mtu.”

Haambiliki, jina ambalo halikumea sana kama mengine aliyopachikwa kiongozi huyo yakiwamo; Mzee Kifimbo (kutokana na kubeba fimbo yake mara zote) na Mchonga Meno (kwa kuwa na meno yenye ncha), lakini lilisikika kwa baadhi ya watu na hata mwenyewe aliwahi kukiri kulitambua, huku akisema “watu walinieleva vibaya kwa msimamo wangu.”

Baadhi ya uasi wa Mwalimu Nyerere ni pamoja na kuasi kutii kila amri na “ushauri” wa Wazungu – hasa kutoka taasisi kubwa na mashirika ya fedha ya dunia, ikiwamo Benki ya Dunia (WB)



Mwl. JK Nyerere

ambayo mara zote yalikuwa yakishauri namna ya “kuboresha uchimi,”

Mwalimu hakuwa mwepesi kufuata ushauri wao, kwani aliamini wao, kwa kiasi kikubwa ni wafanyabiashara, ambao masharti yao na ushauri wao, huumiza wananchi kutoka nchi masikini zinapolazimishwa kuchukua mikopo au misaada.

Ni Mwalimu Nyerere aliyekataa ushauri wa wakoloni – baada ya uhuru kwamba Tanganyika isiye mfumo wa maisha na uchumi (ujamaa) kutoka China. Mwalimu hakusikiliza, akaja na mfumo wa Ujamaa na Kujitegemea.

Katika lugha, Mwalimu aliasi matumizi makubwa ya Kiingereza, akaja na sheria ya kutumia Kiswahili, lengo likiwa ni kuunganisha jamii nyingi, tena zikiwa na makabila mengi, kuwa nchi moja yenye kuelewana na kuheshimiana kupitia lugha moja kubwa – ya itaifa.

Mwalimu aliasi ushauri wa kuanza kuchimba madini na kuvunwa kwa maliasili zingine za thamani. Hakuwakubalia matajiri wa nchi za magharibi waliokuwa wakimshawishi kwamba “umasikini wa Tanzania na watu wake, utapunguzwa kwa kiasi kikubwa na madini hayo.”

Kiongozi huyo wa Tanzania na mwana aliyetukuka wa Afrika, Mwalimu Nyerere, alitenda uasi chanya wenye manufaa ambao leo tunaushuhudia kupitia misingi ya uongozi na utendaji aliyoweka, hata kama waliomfuatia walivuruga.

Aibu wabunge kushindwa uwaziri

Na Dkt. Bullet RUHINDA

Kumekuwa na kelele nyingi za wazi na za kificho za kutaka katiba mpya.

Sababu ni nyingi, lakini kubwa zimekuwa kwamba katiba ya sasa ilitengenezwa kwa taswira ya nchi ya chama kimoja. Lakini pia kwamba katiba iliyopo haina majawabu ya matatizo mengi ya sasa.

Kwa kifupi, katiba iliyopo haiendani na wakati tulionao.

Pamoja na kelele hizo za kuhitaji katiba mpya, zipo pia kelele kinzani ambazo nazo pia zinatoa hoja zake, mfano mchakato wa katiba ni gharama, pia kwamba wananchi wanahitaji maendeleo na siyo katiba.

Kwa hili nashawishika kuwauliza wapiga kelele kinzani wa katiba mpya kama kuna uhusiano wa katiba na maendeleo. Jibu lao litaweza kutoa mwanga kama katiba ni muhimu au siyo muhimu.

Pamoja na kwamba mimi siyo mwanasheria, bado kwa upeo wangu, ninaona kuna shida kidogo katika eneo la mawaziri watokanao na wabunge wa kuteuliwa.

Katiba inaongoza kwamba katika uchaguzi mkuu tunawapata rais, wabunge na madiwani. Baada ya uchaguzi rais anaweza kuteua mpaka wabunge kumi kwa nafasi yake.

Kwa maana hiyo, uchaguzi unatupatia wabunge zaidi ya 300 waliochaguliwa moja kwa moja na wananchi. Pia wabunge 10 waliopatikana kwa matakwa ya rais.

Ni katika wabunge hao ndio tunalipata baraza la mawaziri. Rais anao uchaguzi mkubwa wa kupata mawaziri waliotokana na kura za wananchi.

Endapo wateule wake hao (waliotokana na kura za wananchi) hawataweza kufanya kazi yenye tija, wananchi wanaweza kulaumiwa kwa kumchagulia rais wabunge wasioweza



Spika Dk. Tulia Ackson

kazi ya uwaziri.

Lakini kwa katiba hii tuliyonayo ambayo inampa madaraka rais - ya kuteuwa wabunge kumi anaopenda yeye na kuwapa nafasi za uwaziri kama anavyotaka yeye (kasoro waziri mkuu), ina walakini.

Kwa sababu wabunge wasiopigiwa kura na wananchi wanateuliwa kufanya kazi ambazo kwa hakika zilitakiwa kufanywa na watu waliopigiwa kura.

Wabunge wa aina hiyo hawana ukaribu na wananchi bali rais, maana ni wateule wake. Utendaji kazi wao (inawezekana siyo mara zote), utakuwa wa kumpendeza aliyewateua badala ya wananchi ambao ni wapiga kura.

Endapo hawatafikia matarajio ya kazi waliyopewa, bado wananchi hawatapata mtu wa kumlaumu, maana "rais halaumiwi!" Itabaki rais anajilaumu mwenyewe kwa wateule wake bila ushirika wa lawama kutoka kwa wananchi.

Ingekuwa vyema kwamba pamoja na mamlaka aliyonayo rais ya kuteua mawaziri, basi awapate kutoka kwa wale waliopigiwa kura maana ni wengi zaidi ya 300!

Ni aibu wabunge zaidi ya 300 waliochaguliwa kushindwa kujaza nafazi za baraza la mawaziri. Mabadiliko madogo katika baraza la mawaziri yaliyofanyika Oktoba 2, 2022 yanaakisizi vizuri mkanganyiko huu.

Pennyroyal wakomaa kusaka haki

Na Jabir Idrissa

MKATABA wa ushirikiano wa Kibiashara kati ya Tanzania na Uingereza uliosainiwa mwaka 1994 sasa unatumika kutafuta suluhu ya kilichoibuka kuwa mgogoro kati ya wawekezaji kutoka Uingereza na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Huo ni mkataba unaotambuliwa kama “Makubaliano ya Kuendeleza na Kuhifadhi Miradi ya Kibiashara ya Wananchi” wa pande hizo mbili ambao ulisainiwa Januari 7, 1994 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Uingereza na utekelezaji wake kuanza rasmi Agosti 1996.

Kwa mujibu wa mkataba huo, migogoro inayotokea ikishindikana kutatuliwa kwa mazungumzo, itapaswa kuwasilishwa kwa njia ya kesi kwenye Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji na Biashara - International Centre on the Settlement of Investment Disputes (ICSID).

Mkataba unalenga kuipa uhakikisho wa ulinzi na hifadhi miradi ya uwekezaji inayowekwa na nchi hizo mbili pamoja na raia wake dhidi ya kuhujumiwa kwa kutaifishwa, kufiliwa au kwa namna nyinginezo.

Hatua hii imekuja sasa baada ya wamiliki wa kampuni ya Pennyroyal Limited ya Uingereza “kuishitaki” Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) kuhusu uamuzi wake wa kusitisha leseni ya ukodishaji wa eneo la uwekezaji lenye ukubwa wa hekta 411 lililopo kijijini Matemwe, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Kwenye eneo hilo tayari kuna shughuli mbalimbali za ujenzi wa majengo yaliyokusudiwa kwa vitegauchumi ikiwemo hoteli za kisasa za kitalii; nyumba za kuishi watu; eneo la kuchezea gofu na la kuonesha burudani ya boti za kifakhari (yatch), na tayari nyumba kadhaa zimeshapata wanunuzi.

Baadhi ya wanunuzi wameeleza kushtushwa na walichoeleza na



Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Mwinyi

wanajiuliza vipi hatua kama hiyo ichukuliwe wakati uwekezaji mkubwa wa mamilioni ya dola umefanyika na hakukuwa na mgogoro wowote.

“Hivi mimi jitihada zangu zote za kuhangaikia kupata nyumba ya kuja kuishi Zanzibar ninapostaafu kazi, ndio zinafikishwa kilele cha namna hii. Itakuwaje sasa zile fedha zangu kiasi kikubwa nishalipa kumiliki nyumba?” Ni kauli ya Mwingereza ambaye amebakiza malipo ya “asilimia cache tu” ya malipo ya Dola za Marekani 450,000 kununua nyumba moja kwenye eneo hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Pennyroyal Limited, Brian Thomson amethibitisha taarifa kwamba ameiarifua SMT nia yake ya kufungua kesi kwenye mahakama hiyo iliopo jijini London, Uingereza kupigania haki yake.

Amewasilisha tishio la kuishitaki SMT kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi.

Pennyroyal inayojinasibu kuwa na vibali vyote kwa mujibu wa taratibu za kisheria zinazosimamiwa na Mamlaka ya Uwekezaji ya Zanzibar (ZIPA), inadai kutumia Sh. 126 bilioni kuwekeza kwenye eneo la Matemwe, Zanzibar kupitia mradi unaosimamiwa na Blue Amber Resort ambao ukikamilika kulingana na makisio, utagharimu Sh. trilioni 3.

Wanajeshi wantikisa Nyerere

Na Waandishi WETU

PAMOJA na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuwa na sifa zilizotukuka wakati wa harakati za kudai uhuru, kupatikana kwa uhuru na uongozi wake wa miaka 24 akiwa Rais wa Tanzania, alitikiswa mara kadhaa.

Mtikisiko wa kwanza wa uongozi wake ulianza Dar es Salaam, kutoka kwa wanajeshi waliokuwa Kambi ya Colito (sasa Lugalo) ambao, pamoja na wenzao kutoka kambi nyingine mbili, walipanga njama za kumuua na kuondoa madarakani uongozi wake.

Wanajeshi hawa hawakufurahishwa na baadhi ya mambo katika uongozi wake na pia kudai nyongeza ya maslahi yao – kwa kuamini wao walipaswa kupata zaidi ya wanasiasa.

Misingi ya uongozi ya Mwalimu Nyerere ilijengwa katika usawa, uhuru na umoja na kwamba ni dhana zinazounda pembetatu ya mfumo wa tunu zilizo msingi wa falsafa ya “ujamaa” iliyoipiganiwa zaidi na Mwalimu Nyerere, muasisi wa Tanganyika na baadaye Tanzania tangu Aprili, 1962.

Mwalimu Nyerere aliweka bayana

msimamo wake kwenye makala yenye kichwa cha maneno, “Ujamaa: Msingi wa Maisha ya Afrika,” aliyoiandaa kwa ajili ya chama chake cha TANU.

Hata hivyo, ndani ya miaka miwili pekee ya Uhuru wa Tanganyika, yaani Januari 19, 1964, falsafa ya “ujamaa” ilitikiswa na wanajeshi waasi kutoka Jeshi la Tanganyika, yaani “Tanganyika Rifles.”

Uasi wa “Jeshi la Tanganyika” ulitokea siku saba tu baada ya Mapinduzi ya Zanzibar - ya Januari 12, 1964. Uasi huu ulidumu kwa siku saba, tangu Januari 19 hadi Januari 25, 1964.

Wanajeshi waliohusika walitoka Kambi ya Jeshi ya Lugalo ya Dar es Salaam, Kambi ya Jeshi ya Tabora, na Kambi ya Jeshi ya Nachingwea. Kiongozi wa uasi huo alikuwa Sajenti Francis Hingo Ilogi, wa Kambi ya Jeshi ya Lugalo, Dar es Salaam.

Wanajeshi waasi walikuwa katika mgomo wa kikazi, wakitaka kuanzishwa kwa sera ya uwezeshaji wa wazawa wa Afrika, sera ambayo ingehakikisha kwamba nafasi za juu jeshini zinashikwa na Waafrika badala ya kushikwa na Wazungu.

Inaendelea Uk. 10



Baraza la Kwanza la Mwalimu Nyerere: Mbele kutoka kushoto: Waziri wa Serikali za Mitaa, Job Lusinde; Waziri asiyekuwa na wizara maalum, Rashidi Kawawa; Waziri wa Biashara na Viwanda, Nsilo Swai; Waziri wa Elimu, Oscar Kambona; Waziri wa Ardhi, Misitu na Wanyamapori, Tewa Saidi Tewa; Katibu wa Baraza, Charles MEEK. Mbele kutoka kushoto: Waziri wa Kilimo, Paul Bomani; Waziri wa Sheria, Abdallah Fundikira; Waziri Mkuu, Julius Nyerere; Waziri wa Fedha, Ernest Vasey; Waziri wa Mawasiliano, Nishati na Ujenzi, Amir Jamal. Asiyekuwapo kwenye picha ni pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani, George Kahama. (Picha imechukuliwa kutoka MAELEZO).

Nani anagawa madaraka ? - 1

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

SWALI kwamba – “nani hasa anagawa madaraka,” limekuwa gumu katika kulijadili na hata kutekeleza kwa vitendo ukweli wake.

Ugumu huu hujitokeza zaidi katika mataifa ambayo mifumo yake ya utawala siyo ya kidemokrasia; hakuna utawala bora; hakuna uwajibikaji ipasavyo; kuna uminywaji wa haki za binadamu; na utawala wa sheria unayumbayumba.


Nikiri kwamba tunu hizo zinazopima ubora wa jamii ya kisiasa, zipo kwa uwiano tofauti katika mataifa mbalimbali. Kwa maana hiyo, wapo ambao wamefanikiwa kujenga miundo na mifumo ambayo iko juu na wengine chini kabisa.

Napingana kabisa na wale wanaodai kwamba tunu hizo hazifai kwa mataifa ya Afrika. Kusema hivyo ni sawa na kushabikika udikteta. Ukweli ni kwamba tunu hizi hulinda ubora wa maisha na uhuru na furaha ya watu katika taifa.

Hudhihirisha utashi wa hiari wa kutendeana haki ili kudumisha amani ya jamii. Jambo la kushangaza ni kwamba wale wanaozipinga tunu hizo mara nyingi ni watawala na maswahiba wao. Watu hao hawajawahi kutengeneza mfumo mbadala unaofaa kwa mataifa ya Afrika (au mengineyo). Badala yake tunashuhudia kwa vitendo vyao vya kikati kwa wale wanaothubutu kuishi kwa uhuru.

Wakati mwingine dunia inashuhudia michakato ya kuandika katiba na sheria zinazolinda tunu hizo za utawala kufanyika kwa kasi zaidi kuliko utekelezwaji wake. Inatokea hivyo hasa pale ambapo katiba na sheria hizo hazikuminya nguvu wanazopewa watawala.

Mara nyingine kumekuwa pia na kusita kukubali mabadaliko ya katiba na sheria hizo ikiwa mabadiliko hayo yanawapunguzia watawala nguvu walizonazo. Kwa kawaida nguvu hudai



Mwl. Nyerere

nguvu zaidi ili kujilimbikizia nguvu zaidi na kujilinda.

Hivyo kumekuwa na mivutano katika mataifa mengi baina ya watawala wa watawaliwa juu ya umiliki wa taifa na kiini/kitovu cha nguvu na madaraka.

Kwa hiyo swali hili juu ya nani anagawa madaraka na mgawanyo wa madaraka yanashabihiana sana. Mara nyingi migogoro ya kisiasa ina asili katika mambo haya. Hii inatokana na kwamba wanaotoa madaraka na wanaopewa madaraka - kila mmoja anashindwa kusimama katika zamu yake.

Inakuwa hivyo kwa njia mbili. Kwanza; kwa sababu katiba na sheria zinakuwa mbaya kiasi kwamba haiko wazi kuwa nani ana madaraka na ndiye anayeyagawa kwa wengine. Pili; kwamba katiba na sheria zipo lakini usimamiaji na utekelezwaji wake ni dhaifu. Kwa hali hizo waliokabidhiwa madaraka wamejinyakulia na kujilimbikizia madaraka hayo na kutumia hata nguvu za dola kujilinda madaraka hayo.

Vilevile tukumbushane kwamba aina ya watu katika jamii ni muhimu katika kuonyesha itikio kwa hali hizo mbili zilizotajwa hapa. Kama nilivyowahi kusema – watu wawajibikaji ipasavyo hutengeneza jamii inayowajibika ipasavyo.



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Viongozi waepuke kauli hatarishi

KILA wiki nimekuwa nikichapisha kwenye blogu yangu iitwayo “Ujasusi Blog” taarifa kuhusu matukio ya ugaidi nchini Nigeria (kila Jumatano) na sehemu mbalimbali duniani (kila Ijumaa).

Japo lengo kuu ni kuhabarisha, taarifa hizo pia hunisaidia kufahamu yanayojiri katika nchi mbalimbali duniani. Na kila mara hutamani Watanzania wenzangu wafahamu kwamba licha ya changamoto mbalimbali zinazoikabili nchi yetu, tuna bahati kubwa ya kuwa na amani.

Ninatambua fika kuwa neno “kuwa na amani” linaweza kuzua mjadala mwingine, ambapo yawezekana kuibuka hoja kama “kuna amani gani kama sina uhakika wa mlo wa kesho?”

Lakini kwa minajili ya makala haya, “kuwa na amani” kunaangaliwa kwa kulinganisha na yanayojiri nchi kama Jamhuri ya Kidemokrasia Ya Kongo, Msumbiji, Somalia, Ukanda wa Sahel, na maeneo mengine ambako kumegubikwa na wimbo la ugaidi.

Ni katika mantiki hiyo, matukio mawili yaliyojiri huko Tanzania siku chache zilizopita yaligusa hisia zangu kuhusiana na suala la ugaidi na amani.

Katika tukio la kwanza, Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Tunduru alikiandikia barua Chama cha ACT-Wazalendo kukifahamisha kuwa ombi lao la kufanya ziara ya Katibu Mkuu wa chama hicho wilayani humo, limekataliwa kutokana na kuwepo matishio ya ugaidi.

Licha ya ukweli kwamba uamuzi huo wa jeshi hilo ulilenga kukandamiza haki za kidemokrasia na kikatiba za ACT-Wazalendo, pia una athari kwenye jitihada za Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kukuza utalii, hususan kupitia filamu ya ‘Royal Tour.’ Polisi wanaposema kuna tishio la ugaidi nchini ni kama wanawatahadharisha watalii “msije Tanzania, kuna ugaidi.”



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson

Tukio jingine la kusikitisha ni kauli ya Spika wa Bunge la Muungano, Tulia Ackson, aliyoitoa kwa vijana wa CCM, kwamba “akitokea mtu yeyote nje au ndani ya chama hicho akimsema vibaya Rais Samia, “shughulika naye.”

Spika Tulia ni mwanasheria kitaaluma. Anafahamu kwa uhakika kuwa endapo mtu atatenda jambo kinyume cha sheria, vyombo vya sheria ndivyo vyenye mamlaka ya “kushughulika na mtu huyo.”

Badala ya “kuwajaza upepo vijana hao wa CCM” Spika Tulia alipaswa kuwaeleza taratibu za kisheria dhidi ya watu “wanaowasema vibaya viongozi” (japo hilo siyo kosa kisheria).

Ni muhimu kwa viongozi wetu na Watanzania kwa ujumla kuepusha kauli zinazoweza kuhatarisha amani iliyopo nchini mwetu.

Wanajeshi wantikisa Nyerere

Baada ya uchunguzi wa kina, vyombo vya usalama vilibaini kuwa, kwa ajili ya kufanikisha dhamira yao, tayari wanajeshi waasi walikuwa wamekwishaandaa orodha ya majina viongozi wa serikali waliopaswa kuuawa.

Pia waasi walikwishaandaa orodha ya viongozi wa Baraza Jipya la Mawaziri. Waasi hawa walipanga kutekeleza mapinduzi kati ya tarehe 25 na 26 Januari, 1964.

Kwa ajili ya kulinda heshima ya Tanzania kama Taifa ambalo ni “kisiwa cha amani,” serikali ya Tanganyika ililazimika kufanya majadiliano na wanajeshi waasi. Kupitia majadiliano hayo, serikali ilikubali baadhi ya matakwa ya waasi, na hatimaye wakamaliza mgomo na kurudi kambini.

Lakini, Mwalimu Nyerere hakuwaamini tena wanajeshi hawa. Hivyo, aliomba msaada wa vikosi vitatu vya makomandoo wa Uingereza. Vikosi hivi vilitua kwenye Kambi za Jeshi za Lugalo, Tabora na Nachingwea, na kufanikiwa kuwapokonya silaha wanajeshi waasi. Hatimaye waasi wote walifukuzwa kazi na kurudishwa vijijini kwao.

Katika kuhitimisha mnyukano wa siku saba kati ya waasi na serikali, Nyerere alitoa hotuba murua kwenye hafla ya chakula cha jioni, kilichoandaliwa na Taasisi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa - “Dag Hammarskjold Foundation,” jijini Dar es Salaam.

Hotuba ya Nyerere ilikuwa na kichwa cha maneno “The Courage of Reconciliation,” yaani “Ujasiri wa Kufanya Maridhiano.”

Katika hotuba hii, Nyerere alimreja mwanafalsafa wa Kiingereza, John Locke, kuhusu mtazamo wake bora juu ya “nadharia ya mwafaka wa kitaifa” kama msingi wa dola imara na yenye amani.

Wiki mbili baada ya kazi ya kuwapokonya waasi silaha kukamilika, Nyerere alifanya mageuzi makubwa ya kitaasisi ndani na nje ya jeshi.

Mosi, Nyerere alimpumzisha kazi

Brigedia Douglas, na kumteua Mrisho Sarakikya kuwa Mkuu wa Majeshi mpya.

Pili, watu wapatao 500 walikamatwa, kuhojiwa, kushitakiwa na kufungwa, kwa miaka tofauti.

Tatu, Nyerere alivunja chama cha wafanyakazi cha TFL, na kuunda “The National Union of Tanganyika,” yaani NUTA, iliyowekwa chini ya Wizara ya Kazi.

Nne, Nyerere alianzisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Jeshi la Mgambo, na Jeshi la Wananchi wa Tanganyika (JWTZ) lililochukua nafasi ya Tanganyika Rifles.

Na tano, Nyerere alianzisha Jeshi la Makomandoo, kwa ajili ya kuondoa usumbufu wa kuwaazima kutoka ng’ambo kama ilivyotokea mwaka huo wa 1964.

Mchakato wa kuliunda upya Jeshi la Tanganyika ulifanyika kwa msaada wa wataalam wa kijeshi kutoka Nigeria, Algeria, Ethiopia, Uingereza na China.

Kwa ufupi, maasi haya yalikuwa ni fursa kwa Nyerere kuonyesha uwezo wake akiwa kiongozi wa taifa changa, mwenye jukumu la kuweka misingi thabiti ya mamlaka kamili ndani ya mipaka ya nchi inayoongozwa kwa mujibu wa dira ya utu, na yenye kutambulika kimataifa.

Hata hivyo, maasi ya “Jeshi la Tanganyika” ya mwaka 1964, na jinsi yalivyoshughulikiwa yalizusha gumzo za aina tofauti kulingana na mleta gumzo.

Baadhi walisema kwamba, vurugu za kijeshi ni ushahidi kwamba, bila msaada kutoka nje, Waafrika hawana uwezo wa kujiongoza. Wengine walisema kuwa, Waafrika wanapenda sana kutumia mabavu kutafuta madaraka badala ya kutumia njia za kidemokrasia.

Na kuna waliosema kuwa vurugu hizo ni ushahidi kuwa makoloni yalipewa uhuru wa bendera tu, kwani wakoloni bado wanaendesha nchi hizo kupitia mlango wa nyuma.

Uchambuzi ufuatao, wenye kuonyesha matukio yote muhimu tarehe kwa tarehe, unabainisha jinsi Nyerere alivyofanikiwa

Wanajeshi wantikisa Nyerere

kuzima jaribio la mapinduzi na hatimaye kurejesha heshima ya Tanzania kama kisiwa cha amani.

Matukio kabla ya Januari 19, 1964

Mara tu baada ya uhuru, Desemba 9, 1961, Nyerere aliteua Baraza la Mawaziri la kwanza, likijumuisha Waafrika, Waasia na Wazungu.

Jambo hili liliakisi Imani ya Nyerere kuhusu usawa wa tabaka la bindamu, bila kujali tofauti za rangi zao. Lakini, tangu siku ya uhuru, kulikuwa malalamiko makubwa matatu jeshini.

Mosi, ni uwepo wa wageni wengi katika nafasi za juu za uongozi. Hivyo, Waafrika walitaka kuanzishwa kwa Sera ya Uwezeshaji wa Wazawa ambao ni Waafrika.

Lakini, sera hii haikuwa inakubalika kwa Nyerere. Mnano Januari 1964, Nyerere alipiga marufuku sera hiyo nchini, kwani ilikuwa kinyume na itikadi ya usawa wa binadamu, aliyokuwa anaisimamia kama mkuu wa nchi.

Badala yake, Nyerere alitangaza kuwa, “nafasi zote za uongozi zijazwe kwa kutumia kigezo cha uraia pekee, bila kujali rangi ya ngozi.”

Pili, jeshini kulikuwa na ubaguzi katika mfumo wa mishahara. Wakati huo, mishahara ulianzia shilingi 106 kwa wanajeshi wa ngazi ya “private,” hadi shilingi 460 kwa wanajeshi wa ngazi ya “warrant officer.”

Naye Nyerere, kama mkuu wa nchi, mishahara wake ulikuwa shilingi 3,000 kwa mwezi. Hivyo, kwa wastani, mishahara wa chini wa mwanajeshi ilikuwa sawa na asilimia tatu ya mishahara wa Rais.

Na tatu, wanajeshi walilalamikia ubaguzi kwenye huduma ya bure ya nyumba. Hapa, wanajeshi Waafrika wenye cheo sawa na Wanajeshi Wazungu, walikuwa wanapewa nyumba zenye hadhi tofauti.

Wakati Waafrika kadhaa walikuwa wanashirikiana nyumba moja, wanajeshi wa Kizungu wa cheo sawa na wanajeshi

wa Kiafrika, hawakuwa wanashirikiana nyumba. Kila mmoja alikuwa na nyumba yake.

Matukio ya Jumpili, Januari 19, 1964

Jioni ya Januari 19, 1964, yaani, wiki moja tu baada ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyotokea Januari 12, 1964, Nyerere aliandaa tafrija Ikulu, akawaalika mabalozi na viongozi wa Zanzibar ili kujadili upepo wa kisiasa huko Zanzibar, na matumaini ya Zanzibar mpya, baada ya vurugu za umwagaji damu zilizoongozwa na chuki za kimbari.

Wakati gumzo za vijiwani zikiwa bado zinahusu mapinduzi za Zanzibar, baadhi ya wanajeshi katika Kambi ya Lugalo, karibu na Mwenge, Dar es Salaam, waliona ni busara kutumia fursa hiyo kutambulisha malalamiko yao kwa jamii pana.

Wanajeshi hawa walianzisha mgomo kazini. Kwa kuwa wanajeshi ni watumishi wa umma wenye silaha, mgomo wao haukuwa na uzito sawa na mgomo wa kikazi wa watumishi baki wa umma. Na kweli, baadaye mgomo huu uliungwa mkono na wanajeshi wenzao wa Kambi ya Nachingwe na Kambi ya Tabora.

Matukio ya Jumatatu, Januari 20, 1964

Jumatatu ya Januari 20, 1964, saa 7.30 usiku, mwasi mmoja wa kijeshi alipiga kengele ya kuashiria moto kwenye kambi ya Jeshi ya Lugalo, iliyoko Mwenge, Dar es Salaam. Mara, wanajeshi waasi wakaiteka kambi.

Wakawaamsha na kuwafungia kwenye stoo viongozi wao, wengi wakiwa Wazungu. Wakakata nyaya za mawasiliano ya simu. Na vikosi maalum vikaziba na kulinda barabara zote zinazoingia na kutoka kambini. Kisha wanajeshi waasi waliingia barabarani na kuyatwaa maeneo kadhaa ya jiji.

Mnamo saa 9.00 usiku, Makamu wa Rais, Rashid Kawawa, alipata taarifa za uasi huo. Alimwamsha Nyerere, wakajadiliana, na baadaye Kawawa

Wanajeshi wamtikisa Nyerere



Mwalimu Nyerere akikagua Gwaride la Heshima alipowasili New Delhi, India 25 Agosti 1985.

akaelekea kwenye Kambi ya Jeshi ya Lugalo.

Na baadaye kidogo, usiku huo huo wa kuamkia Jumatatu, baadhi ya wanajeshi waasi, wakiwa wamevaa mavazi ya kivita, walifanikiwa kufika Ikulu ya Magogoni, na kuizingira Ikulu. Walibisha hodi mlangoni, kwenye makazi ya Rais Nyerere, wakafunguliwa, na kumkuta Maria Nyerere na watoto wake pekee.

Tayari Nyerere alikwisha kuhamishwa na Kikosi cha Usalama wa Rais, kupitishwa eneo la bandarini, na kufichwa kwenye Parokia ya Kanisa Katoliki, huko Kurasini, Dar es Salaam.

Taarifa hizi ni kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2015, uliofanywa na Paul Bjerck, na kuandikwa kwenye kitabu chake, "Building a Peaceful Nation."

Kwa mujibu wa utafiti wa Paul Bjerck, Kiongozi wa Kikundi cha wanajeshi waasi kilichokuwa kinatetemeshwa Jiji alikuwa ni Sajenti Francis Hingo Ilogi.

Chini ya uongozi wa Sajenti Ilogi, hadi alfajiri ya Jumatatu, wanajeshi waasi walikuwa tayari wameteka Ikulu, uwanja wa ndege, kituo cha polisi, Ofisi za Makao Makuu ya Posta na Simu, kutwaa kituo cha utangazaji cha Taifa (TBC), na kuwaweka chini ya ulinzi wanajeshi

wa Kizungu waliokuwa viongozi wakuu jeshini, akiwemo Mkuu wa Majeshi, Brigedia Douglas.

Siku hiyo, Sajenti Ilogi aliandika telegram kwenda Kambi ya Jeshi ya Tabora akiwaalika waungane kwenye uasi.

Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa wa wakati huo, Emil Mzena, aliweka mpango wa kutafuta mwafaka na kikosi cha waasi, kilichokuwa kinaongozwa na Sajenti Ilogu.

Oscar Kambona, wakati huo akiwa ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ulinzi, alikabidhiwa jukumu hilo. Kambona alikuwa anayaelewa malalamiko ya wanajeshi, maana tangu mwanzo yeye aliibeba sera ya uwezeshaji wa wazawa.

Katika majadiliano yaliyofanyika, wanajeshi waasi walipendekeza Elisha Kavana awe Mkuu Mpya wa Majeshi, na Msaidizi wake mkuu awe Sajenti Ilogu.

Kambona alirudi Ikulu, lakini hakufanikiwa kukutana na Nyerere, wala kuwasiliana naye. Hivyo, baada ya kushauriana na Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Emil Mzena, aliwatangaza mwenyewe hao viongozi wabaya wa jeshi.

Wanajeshi wamtikisa Nyerere

Saa 4.00 asubuhi, Kambona alimwita Balozi wa Uingereza na kumwambia kuwa anakusudia kuwahamisha Wanajeshi wa Kiingereza kutoka Tanzania kwenda Kenya, kwa sababu ya usalama wao.

Katika muda huo, Mkuu wa Kitengo cha Usalama wa Rais, Wynn Jones Mbwambo, aliandika telegram kwenda balozi zote kuwataarifu juu ya hali ya usalama nchini, akieleza utayari wa serikali kujadiliana na waasi. Akawatata watulie.

Hadi saa sita mchana, Wanajeshi wa Kizungu walikuwa wanapakiwa kwenye malori na kukimbizwa uwanja wa ndege. Wanajeshi 30 wa kizungu walipelekwa Kenya, familia zao zikifuata baadaye.

Baadaye mchana huo, serikali ilionekana “kufufuka” polepole. Jeshi la polisi, lenye utifu kwa serikali, liliingia mitaani na kuwakabili vijana waliokuwa wanafanya uporaji kwenye maduka. Wananchi waliamriwa kukaa ndani, na yeyote aliyekaidi amri hiyo alikamatwa.

Saa 7.00 mchana, Waziri Kambona alilihutubia Taifa kwa njia ya redio, na kusema kwamba, tofauti zilizojitokeza kati ya Wanajeshi wa Kiafrika na wanajeshi wa Kizungu kwenye Kambi ya Jeshi ya Lugalo, jijini Dar es Salaam, zimekwisha, na sasa wanajeshi wamerudi kambini.

Mpaka wakati huo, sauti ya Nyerere haikusikika popote, na hata Waziri Kambona hakulitangazia Taifa Nyerere alikuwa wapi.

Kwa sehemu kubwa, wanajeshi waasi waliendelea kushika usukani wa Jiji la Dar es Salaam. Walitangaza amri ya kutotembea usiku. Wakawa wanazunguka mitaani wakivuta bangi hadharani, na kuwasumbua wananchi, hawa wageni.

Matukio ya Jumanne, January 21, 1964

Usiku wa kuamkia Jumanne, Januari 21, 1964, ulipita kimyakimya, huku waasi wakifanya doria maeneo muhimu jijini Dar es Salaam.

Jumanne asubuhi, baadhi ya mawaziri walifanya ziara jijini, ili kuonyesha kuwa serikali ilikuwa kazini. Pia, polisi walizunguka wakiwakamata vijana waliokuwa wanafanya uporaji na kutawanya makundi ya wahuni.

Siku hiyo, taarifa zilipatikana kusema kuwa Batalioni ya Kambi ya Jeshi Tabora ilithibitika kuwa katika uasi. Huko nako, viongozi wa jeshi, wengi wao wakiwa Wazungu na waafrika wachache, walifungwiwa kwenye stoo. Aidha, Batalioni ya Kambi ya Jeshi Nachingwea ilikuwa imeasi tangu alfajiri.

Kwa mujibu wa kauli ya Sajenti Ilogi, baada ya Kambona kusikia taarifa za uasi wa Tabora, alifanya mashauriano naye, na wakakubaliana ateliwe Mwafrika kuongoza Kambi hiyo. Kambona alimteua Kapteni Mrisho Sarakikya, kuongoza Kambi ya Jeshi ya Tabora.

Sarakikya aliwapa ulinzi wanajeshi wa Kizungu waliokuwa wamefungiwa stoo; na kuwaachia huru viongozi wa jeshi waliokuwa Waafrika. Baadaye, wanajeshi wa Kizungu walipelekwa Nairobi. Wakati wanasubiri ndege kwenye uwanja wa ndege wa Tabora, Sarakikya alimweka David Msuguri, kama mlinzi wao.

Kufikia saa 6.00 mchana, matangazo ya TBC yalirudi hewani, likirushwa tangazo la hotuba ya Kambona, kila baada ya nusu saa. Hotuba iliwaonya wahalifu na kuwakumbusha watu kuwa, kilichokuwa kinaendelea sio jaribio la mapinduzi dhidi ya serikali, bali madai ya mishahara bora jeshini.

Hata hivyo, mchana huo kulitokea vurugu kwenye soko la Kariakoo, kati ya waasi na raia waliokuwa wanajaribu kufanya uporaji. Hatimaye, watu wapatao 30 walikufa, na wengine 250 kujeruhiwa.

Katika harakati za kumtafuta mchawi wa uasi, polisi waliwakamata watu kadhaa, wakiwemo Joseph Nyerere, na Bibi Titi Mohamed.

Kwa mujibu wa Balozi wa Uingereza nchini kwa wakati huo, “hadi wakati huo,

Wanajeshi wamtikisa Nyerere

serikali ilikuwa inatekeleza majukumu yake kupitia kwa Oscar Kambona, yenyewe ikiwa nyuma ya pazia”

Akiwa bado amejificha kwenye Misioni ya Katoliki ya Kurasini, Nyerere alirekodi hotuba, akihimiza utulivu, akionyesha huzuni juu ya “aibu iliyolikumba Taifa.”

Hotuba ya Nyerere ilirushwa TBC saa 2.15 usiku. Katika hotuba yake, aliwahakikishia wananchi kuwa tatizo limekwisha, na kwamba sasa watulie na kuchapa kazi.

Usiku huo, Nyerere alirudi kimya kimya Ikulu. Na usiku huo huo Nyerere alikutana na Balozi wa Ufaransa.

Alimfahamisha Balozi wa Ufaransa kwamba, madai ya wanajeshi hayakuwa na chembe yoyote ya kisiasa, badala yake yalikuwa ni madai ya mishahara na upinzani dhidi ya ubaguzi kwenye nafasi za uongozi wa juu wa jeshi, yakiwa yamefanywa na watumishi wa umma wanaomiliki silaha.

Matukio ya Jumatano, January 22, 1964

Jijini Dar es Salaam, siku ya Jumatano, January 22, 1964, ilianza kwa utulivu. Wafanya biashara walifungua maduka yao.

Baraza la Mawaziri lilikutana chini ya Makamu wa Rais, Rashid Kawawa, na likakubaliana kwamba, hali ilikuwa salama kwa ajili ya kumruhusu Rais Nyerere kulitembelea jiji.

Siku hiyo, Rais Nyerere alikutana na Mabalazi na kuwafahamisha kuwa, Mkuu Mpya wa Majeshi, Kavana, aliyependekezwa na kikosi cha wanajeshi waasi, alikuwa ni “mwanajeshi mzuri.”

Hivyo, alitangaza kuwa tayari kufanya kazi naye, na kuongeza kwamba, baada ya hali kutulia, ataangalia namna ya “kuyapalilia magugu ya wanajeshi wasio na sifa na kuwaelimisha wanajeshi juu ya ukubwa wa kosa lao la uasi.”

Matukio ya January 23, 1964

Asubuhi ya Alhamisi, January 23, 1964, serikali ilianza kusafisha uso wake. Nyerere aliongea na maandishi wa habari, na kupitia kwao, akaongea na wananchi



MwLJK Nyerere

wote moja kwa moja kwa njia ya redio.

Alilaani fitina za uwongo dhidi yake na serikali yake kwa sababu “fitina hizo ni hatari kuliko uasi wa jeshi uliokuwa unaendelea,” kwani “zinaufanya uwezo wa serikali na uimara wa nchi kutiliwa shaka,” alisema Nyerere. Hivyo, aliunda kikosi kazi kwa ajili ya kufuatilia chimbuko la fitina hizo na kuviteketeza haraka.

Matukio ya January 24, 1964

Kufikia asubuhi ya Ijumaa, January 24, 1964, utulivu mkubwa ulikuwa umerudi Jijini Dar es Salaam.

Lakini, mpaka siku hiyo, tayari Idara ya Usalama wa Taifa, ilikuwa imegundua mpango wa chama cha wafanyakazi wa kuipindua serikali ya Nyerere.

Ugunduzi huu ulitokana na msako uliofanywa na Idara ya Usalama wa Taifa, kwenye nyumba za viongozi wa chama cha wafanyakazi. Kwa mujibu wa Mkuu

Mwalimu katika barabara ya historia

Na Madaraka NYERERE

JULIUS Kambarage Nyerere, maarufu kwa taji la “Mwalimu,” alizaliwa Aprili 13, 1922 katika kijiji cha Butiama, kilichoko kwenye mwambao wa Ziwa Viktoria, wilayani Musoma, Mkoa wa Mara.

Alikuwa mtoto wa kiume wa Chifu Nyerere Burito wa kabila dogo la Wazanaki. Mama yake, Christina, alikuwa mke wa tano kati ya wake 22 wa Chifu Nyerere Burito.

Mwalimu Julius Nyerere alisoma kwenye Shule ya Msingi ya Mwisenge huko Musoma. Alikuwa anatembea maili 26 kila siku kutoka nyumbani Butiama hadi shuleni na kurudi.

Baadaye alisoma kwenye Shule ya Mt. Mary, iliyokuwa inamilikiwa na Kanisa Katoliki huko Tabora.

Mwaka 1946 alipata stahhada ya ualimu kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, nchini Uganda, na kisha kurudi kufundisha somo la Bayolojia kwenye shule ya Mt. Mary, mkoani Tabora

Mwaka 1949, alikuwa mwanafunzi wa kwanza wa Tanganyika kupelekwa Uingereza, kwenye Chuo Kikuu cha Edinburgh, alikosomea Shahada ya Uzamili katika historia na uchumi. Alihitimu mwaka 1952.

Aliporudi Tanganyika, alipangiwa kufundisha kwenye Shule ya Mt. Francis, iliyoko Pugu, jijini Dar es Salaam.

Akiwa anafundisha hapo, alijiunga na chama cha kijamii kilichoitwa “Tanganyika African Association,” yaani TAA. Wakati huo chama cha TAA kilikuwa hakijasajiliwa rasmi.

Baadaye, chama cha TAA kilibadilishwa jina na kusajiliwa kama chama cha siasa kitaifa kilichoitwa “Tanganyika African National Union,” yaani TANU.

Mwalimu alichaguliwa kuwa Rais wa TANU mwaka 1954, lakini alilazimishwa na wakoloni wa Kiingereza kuchagua kati ya ualimu na siasa. Alichagua siasa ili kuungana na wenzake kukomboza nchi



MwLJK Nyerere

kutoka kwa wakoloni. Aliingia kwa mara ya kwanza katika Baraza la Kutunga Sheria (sawa na Bunge) mwaka 1958.

Desemba mwaka 1961 alikuwa waziri mkuu wa kwanza, baada ya Tanganyika kupata uhuru kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza.

Aprili mwaka 1962, Nyerere aliandika makala katika kijarida yakiwa na kichwa cha habari; “Ujamaa: Msingi wa Maisha ya Kiafrika,” kwa mara ya kwanza akabainisha falsafa yake ya kisiasa kuhusu “utu, usawa, uhuru na umoja,” kama tunu zinazopaswa kuongoza utengenezaji wa sera za nchi.

Septemba mwaka 1962 Tanganyika ilikuwa Jamhuri, Nyerere akachaguliwa kuwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Tanganyika.

Mwaka 1963, Mwalimu alishirikiana na wakuu wa nchi baki za Afrika kuunda Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), uliokuwa na makao yake makuu huko Addis Ababa, nchini Ethiopia.

Aliruhusu Kamati ya Ukombozi ya OAU kuweka makao yake makuu Dar es Salaam. Chini ya mwavuli wa OAU, Mwalimu alikuwa mwenyekiti wa nchi zilizokuwa mstari wa mbele kutokomeza

Mwalimu katika barabara ya historia

Inatoka Uk. 15



Mwl.JK Nyerere

ukoloni barani Afrika.

Aprili, mwaka 1964, Mwalimu alishirikiana na Rais wa Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume kuunganisha Tanganyika na Zanzibar, na hivyo kuunda nchi mpya ya Tanzania.

Mwaka 1967, Nyerere alitangaza Azimio la Arusha. Azimio hilo linasema kwamba, binadamu wote ni sawa; kwamba, kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake; na kwamba, ujamaa na kujitegemea ndio njia pekee ya kujenga jamii ya watu walio sawa na huru.

Kupitia Azimio la Arusha, Mwalimu aliweka msingi wa sera za kitaifa kwa kubainisha tunu za utu, usawa, uhuru, umoja na haki. Mwalimu alibaki muumini wa mafundisho yaliyomo kwenye Azimio la Arusha hadi alipofariki dunia.

Mwaka 1977 aliongoza mabadiliko ya kisiasa kwa kuunganisha chama cha TANU (Tanganyika) pamoja na chama cha ASP (Zanzibar), na hivyo kuunda chama kipya cha Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mwaka 1985 alijiuzulu urais wa Tanzania kwa hiari, baada ya kuiongoza Tanzania kwa miaka 24. Alirithiwa na Rais Ali Hassan Mwinyi kutoka Zanzibar. Lakini alibaki mwenyekiti wa CCM hadi mwaka 1990. Kuanza mwaka 1986 alitekeleza majukumu yake ya kimataifa, kwa kuunda Kamati ya Nchi za Kusini mwa

Sahara, ambazo kwa pamoja zinajulikana kama nchi zenye maendeleo duni ya kiuchumi.

Mwaka 1990, kupitia Kamati ya Nchi za Kusini mwa Sahara, alichapisha ripoti ya “Changamoto ya Nchi za Kusini,” yaani “The Challenge of the South.”

Mwaka 1991 alianzisha Kituo cha Nchi za Kusini mwa Sahara huko Geneva, Uswisi. Kituo hiki kilijihusisha na masuala ya ushirikiano wa kiuchumi na kisera kati ya nchi masikini. Alibaki mwenyekiti wa kituo hicho hadi alipofariki dunia.

Kazi yake ya mwisho katika jukwaa la kimataifa ni kuwajibika akiwa Msuluhishi Mkuu wa Mgororo wa Burundi kwa niaba ya Umoja wa Mataifa, kazi aliyofanya kati ya 1994 na 1999.

Katika viungo vya kimataifa, Mwalimu alikuwa mtetezi wa haki za watu wanyonge, kazi iliyoleta uhasama kati yake na taasisi za kimataifa; yaani Benki ya Dunia (WB), Shirika la Fedha Duniani (IMF), na Kituo cha Biashara Duniani (WTO).

Katika harakati zake za kupinga unyonyaji alioona unafanywa na taasisi hizi, aliwahi kuuuliza: “Tangu lini ‘IMF’ imegeuka kuwa ‘International Ministry of Finance?’”

Mwalimu alifariki Oktoba 14, 1999, kutokana na kansa ya damu (leukaemia) katika Hospitali ya Mt. Thomas, Jijini London, nchini Uingereza.

Nyerere alizikwa kijijini kwake Butiama Oktoba 22, 1999 baada ya kufanyiwa shughuli ya mazishi ya kitaifa jijini Dar es Salaam ambapo viongozi mbalimbali duniani walihudhuria akiwamo Waziri Mambo ya Nje wa Marekani, Medeline Albright, Rais wa Zimbabwe Robert Mugabe, Rais wa Afrika Kusini Thabo Mbeki, Rais wa Uganda Yoweri Museveni, Joaquim Chissano, Uingereza iliwakilishwa na Princess Anne na Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza Peter Hain.

Mwandishi ni mtoto wa Mwalimu Nyerere. Hivi sasa anaishi Butiama.

Matabaka na tokeni zake

Na Deusdedith KAHANGWA

CHARLES Sanders Peirce (1839-1914) pia alifundisha kwamba, wakati kundi la vitu visivyofanana linaunda seti; kundi la vitu vinavyofanana linaunda 'tabaka,' yaani 'type' au 'class,' kwa Kiingereza cha Peirce.

Alifundisha kwamba, wakati vitu vinavyounda 'seti' vinaitwa 'mamba' wa seti hiyo, vitu vinavyounda 'tabaka' vinaitwa 'tokeni' za tabaka hilo, yaani 'tokens,' kwa Kiingereza cha Peirce.

Alifundisha kwamba, wakati ufanano kati ya tokeni za tabaka moja ni chimbuko la umoja wa tabaka, utofauti kati ya tokeni za tabaka moja ni chimbuko la utengano kati ya tokeni hizo.

Alifundisha kwamba, kama ambavyo tunaweza kuwa na 'seti kuu' moja inayogawanyika kwenye 'seti ndogo' kadhaa, kadhalika, tunaweza kuwa na 'tabaka kuu' moja linalogawanyika katika 'matabaka madogo' kadhaa.

Alifundisha kwamba, kwa sababu ya ufanano uliopo kati ya tabaka na tokeni zake, basi, tokeni huwa ni alama inayowakilisha tabaka lake.

Alifundisha kwamba, kama ambavyo tunaweza kuwa na 'seti tupu,' vivyo hivyo, tunaweza kuwa na 'tabaka tupu.'

Na alifundisha kwamba, japo baadhi ya matabaka yanaweza kuwa na sifa za kuitwa seti, sio kila seti inaweza kuwa na sifa za kuitwa tabaka.

Kwa kufundisha juu ya ufanano na utofauti uliopo kati ya tabaka na tokeni zake, Peirce alikuwa amechuja na kuunganisha mawazo ya wanafalsafa waliomtangulia, na hatimaye kuanzisha fani mpya ya kifalsafa itiwajo 'taipolojia,' yaani 'typology.'

Kimsingi, fani ya 'taipolojia' ni tawi la metafizikia linalochunguza na kufafanua ufanano na utofauti uliopo kati ya 'vitu' vinavyounda 'tabaka' moja, vitu ambavyo Peirce anavirejea kama 'tokeni.'

Hivyo, mbali na Peirce kukumbukwa



Charles Sanders Peirce

kama mwasisi wa fani ya 'semiolojia,' yaani 'semiology,' kama tulivyoona hapo awali, pia atakumbukwa kama mwasisi wa fani ya 'taipolojia,' ambayo najadili hapa chini.

Kanuni za taipolojia zinayo matumizi katika sekta kama vile uchumi, lugha, maadili, sheria, siasa, ndoa, ujinsia, na kadhalika. Mifano ifuatayo inatoka kwenye sekta ya sheria.

Katika sekta ya sheria kuna matabaka ya jinai, kila tabaka likiwa na tokeni zake. Hasa, kuna matabaka makuu ya jinai matatu.

Kuna tabaka kuu la jinai dhidi ya watu, tabaka kuu la jinai dhidi ya mali, na tabaka kuu la jinai dhidi ya usalama wa nchi.

Tabaka kuu la jinai dhidi ya watu, lina matabaka madogo saba. Matabaka hayo

Matabaka na tokeni zake*Inatoka Uk. 17*

madogo na idadi ya tokeni zake za uhalifu katika mwaka wa 2021 ni kama ifuatavyo: ubakaji (6,305), mauaji (2,294), ulawiti (1,296), kuiba watoto (58), kutelekeza watoto (149), biashara ya kusafirisha binadamu (25), na kusababisha majeraha ya mwili (0).

Tabaka kuu la jinai dhidi ya mali, lina matabaka madogo 11. Matabaka hayo madogo na idadi ya tokeni zake za uhalifu katika mwaka wa 2021 ni kama ifuatavyo: wizi wa risasi (11), uharamia barabarani (1), wizi wa kutumia silaha (254), wizi wa kutumia nguvu (1,210), wizi wa kuvunja nyumba (9,852), wizi wa kawaida (357), wizi wa bodaboda (4,335), wizi wa magari (155), wizi wa mifugo (3,503), kuchoma moto nyumba (788), na wizi wa fedha (752).

Na tabaka kuu la jinai dhidi ya usalama wa nchi, lina matabaka madogo 16. Matabaka hayo madogo na idadi ya tokeni zake za uhalifu katika mwaka wa 2021 ni kama ifuatavyo: kumiliki silaha haramu (195), kutumia madawa haramu (537), kutumia bangi (7,593), kumiliki mashamba ya bangi (85), na Kati (1,302).

Matabaka mengine madogo ni nyara za serikali (817), kusafirisha madawa haramu (364), rushwa (2), konyagi ya kienyeji (6,022), vifaa vya kutengeneza konyagi ya kienyeji (424), umiliki haramu wa risasi (32), umiliki haramu wa mabomu (6), uvuvi haramu (208), umiliki haramu wa mazao ya misitu (233), umiliki haramu wa mbegu za miti (4), na wahamiaji haramu (1,283).

Kila tokeni ya jinai husika inaambatana na taarifa za lini, wapi, kipivi na kina nani wahusika, na huo ndio utofauti wake na tokeni baki katika tabaka husika.

Kuna matabaka na tokeni zake katika sekta baki kama vile lugha, ambako kuna matabaka ya herufi, maneno na sentensi; sekta ya maadili, ambako kuna matabaka ya matendo adilifu, matendo ya kihalifu, na matendo yasiyofungamana



na upande wowote; na sekta ya uchumi, ambako kuna matabaka ya bidhaa yanayotofautiana kwa sababu ya sifa za bidhaa.

Aidha, kuna matabaka na tokeni zake katika sekta ya siasa, ambako kuna matabaka ya raia yanayotofautiana kwa sababu ya umri wao; sekta ya bayolojia, ambako kuna matabaka ya viumbehai yanayotofautiana kwa sababu ya tabia za viumbehai; na sekta ya ndoa, ambako kuna matabaka ya ndoa yanayotofautiana kwa sababu ya idadi ya wanandoa.

Kadhhalika, kuna matabaka na tokeni zake katika sekta ya ujinsia, ambako kuna matabaka ya matendo ya ngono, kulingana na uwezo wake wa kuleta au kutoleta mimba; sekta ya falsafa ya tunu, ambako kuna matabaka ya tunu; na sekta ya meriolojia, ambako kuna matabaka ya 'vitu vyenye mwili mmoja' yanayotofautiana kwa sababu ya kiunganishi kinacholeta umoja husika.

Wiki ijayo nitajadili 'tabaka la jozi ya watu wanaojamiiana na tokeni zake,' yaani, 'the class of a copulating pair and its tokens,' ambapo kila jozi ya watu wanaojamiiana inatajwa kuwa ni 'mwili mmoja' uliotokana na 'muungano wa watu wawili wanaojamiiana.'

Nitafanya hivyo kulingana na fikra za Aristotle wa Ugiriki ya Kale.

Hujambo!

Ukanushi katika hali ya mazoea

Na Dkt. Michael Mashauri

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuu vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo tunajifunza kuhusu Ukanushi katika hali ya mazoea (Negation in Habitual Tense). Ukanushi huu unafanana na ukanushi wa wakati uliopo. Hujitokeza katika sentensi kama inavyooneshwa katika jedwali. (Negation in habitual tense is similar to negation in present tense. It appears as shown in the table.) -

Examples			
1 st Person	Singular	Affirmative	Mimi huimba wimbo (I always sing a song)
		Negative	Mimi s imbi wimbo (I don't sing a song)
	Plural	Affirmative	Sisi hupika wali kila siku (We cook rice every day)
		Negative	H atupiki wali kila siku (We don't cook rice every day)
2 nd Person	Singular	Affirmative	Weve hulia kila wakati (You cry all the time)
		Negative	Weve h ulia kila wakati (You don't cry all the time)
	Plural	Affirmative	Nyinyi hupenda kucheka (You like laughing)
		Negative	Nyinyi h ampendi kucheka (You don't like laughing)
3 rd Person	Singular	Affirmative	Yeye hupenda kufurahi (He/she likes to be happy)
		Negative	Yeye h apendi kufurahi (He/she doesn't like to be happy)
		Negative	Wao h wali mayai (They don't eat eggs)

Ukanushi katika hali timilifu (Negation in Perfect tense)

Ukanushi katika hali timilifu hutumia ha- na -me- hubadilika kuwa -ja- ambayo hufuata baada ya nafsi – isipokuwa kwa nafsi ya kwanza na ya tatu umoja ambazo hudondosha kiambishi cha nafsi. (Negation in perfect tense uses ha- and -me- changes to -ja- which follows after personal prefix – except for the first and third person singular which drop personal prefix).

Examples			
1 st Person	Singular	Affirmative	Nimekula viazi (I have eaten potatoes)
		Negative	S ijali viazi (I have not eaten potatoes)
	Plural	Affirmative	Tumepika maboga (We have cooked pumpkin)
		Negative	H atujapika maboga (We have not cooked pumpkin)
2 nd Person	Singular	Affirmative	Umeleta nguo (You have brought clothes)
	Negative	H aujaleta nguo (You have not brought clothes)	
3 rd Person	Singular	Affirmative	Amenawa mikono (He/she washed hands)
		Negative	H ajawawa mikono (He/she has not washed hands)

• **Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**

Wanajeshi Wamtikisa Nyerere

wa Kitengo cha Usalama wa Rais, Wynn Jones Mbwambo, mpango huo ulifichua mambo matatu.

Mosi, ni orodha ya viongozi waliopaswa kuuwawa. Pili, ni orodha ya viongozi waliopaswa kuunda Baraza jipya la Mawaziri. Na tatu, ni ratiba kamili ya mapinduzi.

Kwa mujibu wa ratiba ya mapinduzi, hatua ya kwanza ilikuwa ni kuchochea mgomo na uasi ndani ya jeshi. Hatua ya pili ilikuwa ni kuchochea mgomo na uasi ndani ya polisi, ili kupunguza upinzani dhidi ya jeshi.

Hatua ya tatu ilikuwa ni kuchochea mgomo na uasi ndani ya wafanyakazi wa bandari, reli na watumishi wa umma kwa ujumla.

Na nne, ni wanajeshi kumkamata Nyerere na wasaidizi wake, na kisha kuwaua. Kwa mujibu wa ratiba hii, Nyerere na wasaidizi wake walipaswa kuuwawa kati ya tarehe 25 na 26 Januari, 1964

Katika kauli zake za hadharani, Nyerere alitoa matamko ya kidiplomasia. Lakini, nyuma ya pazia alikuwa na mpango wa kijeshi wa kuwapokonya silaha wanajeshi waasi, na kuwaadhibu ipasavyo.

Hivyo, Nyerere aliwatuma wasaidizi wake kuwasiliana na Balozzi wa Uingereza na kuomba Jeshi la nchi yake kumsaidia kuwapokonya silaha wanajeshi waasi, kabla ya Januari 25, 1964, iliyokuwa ni siku yao ya kuipindua serikali. Uingereza ilikubali kutuma kikosi cha makomandoo kwa ajili ya kuwapokonya silaha wanajeshi waasi.

Matukio ya Januari 25, 1964

Alfajiri ya Jumamosi, Januari 25, 1964, wakati Nyerere anatoa hotuba yake kwenye hafla ya pamoja, Kikosi cha Makomandoo wa Uingereza kiliishambulia Kambi ya Jeshi ya Lugalo kwa makombora, kutoka kwenye meli iliyokuwa Bahari ya Hindi. Baadaye kikosi cha makomandoo kilitua kwenye kambi hiyo kwa parachuti.



Mwalimu Nyerere akiwa na Rais Samora Machel wa Msumbiji

Katika muda huo, wanajeshi wakiwa bado wana usingizi, na silaha zao zikiwa bado zimefungiwa stoo, waliamriwa kutembea “mikono juu mwendo wa mateka,” na kisha kukusanyika kwenye uwanja wa mpira, ndani ya saa moja.

Mahali Nyerere alipokuwa anatoa hotuba, sauti ya mizinga ilikuwa inasikika vizuri, lakini, alijifanya hasikii chochote. Akaendelea na hotuba yake.

Saa 7.00 mchana, kikosi cha pili cha makomandoo wa Uingereza kiliingia kwenye kambi ya Jeshi ya Tabora na kuwapokonya silaha, kama ilivyofanyika Dar es Salaam. Na Jumatatu, January 27, 1964, kikosi cha tatu cha makomandoo wa Uingereza kiliingia kwenye kambi ya Jeshi ya Nachingwea na kuwapokonya silaha, kama ilivyofanyika Tabora na Dar es Salaam.

Hapo awali, Jumamosi, Januari 25, 1964, saa 6.00 mchana, Nyerere alihutubia Taifa kuelezea hatua hizo za kijeshi kwenye Kambi za Lugalo, Tabora na Nachingwea.

Sehemi ya hotuba yake ilisomeka hivi: “Kila Taifa huru linayo haki ya kuomba msaada wa kijeshi kutoka nje, kama likiona msaada wa aina hiyo unahitajika.”

Urafiki wa Nyerere na sanaa

Dkt. Vicensia Shule

KUNA mambo mengi ambayo Mwalimu Julius Nyerere anaweza kukumbukwa kwa sababu yake. Moja ya masuala hayo ni jinsi alivyotumia sanaa kueleza falsafa na mawazo aliyokuwa nayo.

Mwalimu alikuwa msanii, mpenda sanaa na mwalimu mzuri. Kwa hiyo, namjadili Nyerere kama msanii na kugusia mipango yake ya kulinda sanaa.

Kwa kutumia ubunifu wake wa kisanii, aliweza kubaini uwezo wa sanaa katika kujenga taifa huru mara baada ya kupata uhuru wake kutoka kwa wakoloni.

Kihistoria, serikali zote mbili za kikoloni za Ujerumani na Uingereza zilikuwa na nia ya kuharibu sanaa ya kuigiza na shughuli nyingine za kitamaduni kwa sababu kwao zilikuwa za 'kishetani' na 'kishenzi'.

Serikali za kikoloni zilipiga marufuku maonyesho mbalimbali ya kimila kutokana na fikra kuwa yana asili ya 'kishenzi'.

Hata hivyo, Nyerere alichukua hatua kadhaa kulinda sanaa. Nazo ni pamoja na: mbio za mwenge wa Uhuru, kuundwa



Mwalimu siku ya kuunganisha udongo wa Tanganyika na Zanzibar.

kwa wizara ya utamaduni, kuanzishwa kwa vikundi vya sanaa vya Taifa (NAGs), tambiko la kuunganisha Tanganyika na Zanzibar, uandishi wa kazi za maigizo, uandishi wa mashairi, Nembo za Taifa, Chuo cha Sanaa Bagamoyo, kuanzishwa kwa Nyumba ya Sanaa, na kuundwa kwa Sera ya Taifa ya Utamaduni.

Baada ya kupatikana kwa uhuru wa bendera usiku wa kuamkia Desemba 9, 1961, Mwenge wa Uhuru uliwekwa juu ya Mlima Kilimanjaro na Alexander

Inaendelea Uk. 22



Mwalimu akicheza bao na wazee wenzake

Urafiki wa Nyerere na sanaa*Inatoka Uk. 21*

Nyirenda ikiwa ni ishara ya kuanza kwa nchi huru. Tangu siku hiyo tuna mbio za kila mwaka za mwenge huo.

Utamaduni huu unaonyesha jinsi Mwalimu Nyerere alivyothamini sanaa ya maonyesho na jukumu lake katika kujenga ufahamu wa watu kuelekea lengo la pamoja.

Nyerere alianzisha Wizara ya Utamaduni na Vijana mwaka 1962. Majukumu yake ni pamoja na kuanza mchakato wa kuwawezesha Watanania kurejesha fahari yao ya kitamaduni.

Nyerere alionyesha wasiwasi wake kuhusu ukoloni ulivyodhalilisha utu wa sanaa za Kiafrika.

Kuanzishwa kwa wizara hii kulikuwa ni mpango wa mwanzo kabisa baada ya uhuru wa kupigana na ubeberu wa kitamaduni.

Nyerere alijua madhara na ukubwa wa ubeberu wa kitamaduni na alichukua hatua za kuushinda kupitia programu mbalimbali za kuondoa ukoloni kupitia sanaa. Program zote zilikuwa zinatekeleza mkakati wa “ukolonuzi wa kifikra,” yaani “mental decolonization.”


Baada ya kuunda wizara hiyo, Mwalimu Nyerere alifanya mageuzi mbalimbali huku akitaka kujenga utamaduni wa taifa kupitia vikundi vya michezo ya kuigiza.

Vikundi mbalimbali vya kisanii vinavyoitwa Vikundi vya Sanaa vya Kitaifa (NAGs) viliundwa pamoja.

Vikundi hivyo vilijumuisha Kikundi cha Taifa cha Ngoma (1963), Kikundi cha Sarakasi cha Taifa (1969) na Kikundi cha Taifa cha Maigizo (1972). Mtazamo wa vikundi hivi ulikuwa katika kukuza umoja wa kitaifa na kutangaza sera za serikali.

Protokali zilizoongoza tukio la kuzindua muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar Aprili 26, 1964, zinaweza kuonekana kama aina ya maonyesho ya kisanii.

Pamoja na utaratibu wa kawaida wa kusaini mkataba na kubadilishana Hati za



Mwalimu akiwa anapiga ngoma

Muungano, Nyerere alichanganya udongo wa nchi hizo mbili.

Nyerere alivaa shati la ngozi ya chui. Alitumia vibuyu viwili vilivyojaa udongo kutoka Tanganyika na Zanzibar. Kisha kuchanganya kulifanyika kwa kumwaga udongo kwenye chungu.

Wanaume wawili walioshika chungu wote walikuwa wamepiga magoti na wamevalia sare ya kitenge maalum kwa ajili ya siku hiyo. Mavazi, vifaa na mchanganyo wa udongo viliashiria jinsi Nyerere alivyothamini sanaa.

Mwalimu pia alitayarisha kazi mbalimbali za maigizo. Kama sehemu ya dhamira yake ya kuondoa ukoloni, Mwalimu alitafsiri tamthilia maarufu za Shakespeare kwa Kiswahili.

Tamthiliya ya “Julius Caesar” ilitafsiriwa

Inatoka Uk. 23

Urafiki wa Nyerere na sanaa

Inatoka Uk. 22

kama “Julius Kaizari” (1968), “Macbeth” ilitafsiriwa kama “Makbeth” (1968) na “The Merchant of Venice” ilitafsiriwa kama “Mabepari wa Venisi” (1969).

Nyerere aliamini kuwa wasomaji wa Kiswahili wanaweza kuelewa vyema maudhui na muktadha wa tamthilia za Shakespeare na kupata fursa ya kulinganisha sanaa za Kiafrika na zilizotoka Ulaya katika mchakato wa kurejesha fahari yao.

Mwalimu pia katika kazi za kiuandishi alitafsiri kwa Kiswahili kitabu cha “The Republic” kilichoandikwa na Mwanafalsafa Plato.

Nyerere pia alitumia ubunifu wa kishairi kushughulikia masuala ya kitaifa yenye utata. Kwa mfano, mwaka 1993 aliandika shairi kuhusu mjadala wa muungano wakati Azimio la Bunge lilipopitishwa kuhusu kuanzishwa serikali ya Tanganyika.

Katika shairi hilo Mwalimu alikuwa akitetea usawa na umoja wa kitaifa na alikuwa akiwapinga viongozi waliotaka kutumia fursa hiyo kwa malengo yao ya kisiasa.

Aidha, Nemo ya Tanzania iliyobuniwa kwa kuwepo ngao ya shujaa katikati ya meno ya tembo iliyowekwa juu ya Mlima Kilimanjaro, inawakilisha ubunifu wa kisanii uliomo katika alama nyingine kama vile bendera, wimbo wa taifa na mwenge wa uhuru.

Ngao ya shujaa inaonyesha vita mbalimbali vya kihistoria vya uhuru. Mwanamume na mwanamke huonyesha heshima kwa usawa wa binadamu bila kujali jinsi, rangi au kipengele kingine chochote cha kijamii.

Mwaka 1981, serikali ilianzisha Chuo cha Sanaa Bagamoyo (BCA); kwa sasa kinajulikana kama Taasisi ya Sanaa na Utamaduni, Bagamoyo au (Tasuba). Kwa njia hii, Nyerere alitaka kuhakikisha uendelevu wa sanaa.

Nyerere alianzisha Nyumba ya Sanaa (nyumba ya wasanii) mwaka 1974.



Mwalimu akiwa amevaa vazi la kitamaduni

Aliamini kwamba ikiweza kutumika ipasavyo, ingepunguza hali ya wasanii kuhitaji kuombaomba kutoka kwa wafadhili na serikali, hali ambayo inawafanya watumwa.

Na sasa, tangu 1997, sera ya kitaifa ya utamaduni imeundwa. Inaeleza umuhimu wa kuanzishwa kwa sanaa, ikiwa ni pamoja na muziki, sanaa nzuri, uchungaji na sanaa za maonyesho, kama masomo ya kutahiniwa katika shule za msingi na sekondari.

• **Tanbihi: Chanzo cha makala haya ni kutoka kwenye chapisho la Chambi Chachage and Annar Cassam (Eds.), Africa’s Liberation: The Legacy of Nyerere, (Kampala, Uganda: Fountain Publishers Ltd, 2010), uk. 160-174. Tafsiri ni yetu-Mhariri.**

PICHA KUBWA



*NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete akifu-
rahia jambo na wapigakura wake wakati wa ziara ya kikazi katika Kata ya Talawa-
nda, Chalinze, mkoani Pwani. Ridhiwani pia ni Mbunge wa Chalinze. Katika ziara
hiyo aliwaasa wananchi kuendelea kushirikiana na serikali kujenga uchumi. (Picha
kutoka Ofisi ya Mbunge Chalinze).*

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa).
Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa
leseni namba - 00000448.

